



CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibucm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiticc@ccmid.in



M/kiti UVCCM: mwenyekituvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

Kumb. Na: CCM/INDIA/007/2026

02/09/2026

RIPOTI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAWI ROBO MWAKA YA PILI – JUNI HADI AGOSTI 2026

1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa wajibu wa kiutendaji wa Tawi la CCM Diaspora – India katika kuimarisha uhai wa Chama, kuunganisha wanachama na wapenzi wa Chama, pamoja na kujenga mifumo madhubuti ya kiutawala na kidijitali, Tawi linawasilisha ripoti hii ya utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha robo mwaka ya pili, kuanzia mwezi Juni hadi Agosti 2026.

Ripoti hii inalenga kutoa tathmini ya hali ya Tawi katika kipindi husika kwa kuangalia mafanikio yaliyopatikana, shughuli zilizotekelezwa, hali ya usajili wa wanachama, mwenendo wa mapato na matumizi, changamoto na mapungufu yaliyobainika, pamoja na mikakati inayopendekezwa kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Tawi katika kipindi kinachofuata.

Kwa ujumla, kipindi hiki kimekuwa cha kujenga misingi ya kiutawala, kidijitali na kiuendeshaji ya Tawi. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado kuna haja kubwa ya kuongeza kasi ya uhamasishaji, usajili wa wanachama, ulipaji wa ada na ushiriki wa viongozi katika utekelezaji wa majukumu yao.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in
Customer care: info@ccmid.in
Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekitilecm@ccmid.in
M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

2.0 MUHTASARI WA UTEKELEZAJI

Katika kipindi cha Juni–Agosti 2026, Tawi limefanikiwa kutekeleza hatua kadhaa muhimu za kimkakati, zikiwemo:

1. Kuanzisha mfumo rasmi wa kidijitali wa Tawi kupitia website rasmi.
2. Kuboresha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za Tawi.
3. Kuendesha mikutano minne ya viongozi kwa ajili ya kujadili na kuratibu shughuli za Tawi.
4. Kuteua viongozi wa mashina ya CCM katika vyuo mbalimbali.
5. Kuwaunganisha wanafunzi wapya wanaoingia India na shughuli za CCM Diaspora – India.
6. Kuanza na kuendeleza usajili wa wanachama wapya kupitia mfumo rasmi wa Chama Cha Mapinduzi kitaifa.
7. Kusaidia wanachama kutekeleza wajibu wa kulipa ada za uanachama.
8. Kuanzisha utaratibu wa kidijitali wa usajili wa wanachama wa Tawi.
9. Kukusanya pamoja wanachama na wapenzi wa CCM katika makundi rasmi ya WhatsApp ya Tawi.
10. Kufikisha idadi ya wanachama waliosajiliwa kwenye mfumo rasmi wa Tawi hadi 33.

Hata hivyo, mafanikio haya bado hayajaendana na ukubwa wa target ya Tawi. Kwa target ya wanachama 200, wanachama 33 waliopo kwenye mfumo wanawakilisha 16.5% pekee ya lengo. Hivyo, kiwango cha usajili bado kiko chini na kinahitaji kampeni kubwa zaidi ya uhamasishaji.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



✉ Admin: admin@ccmid.in
✉ Customer care: info@ccmid.in
✉ Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

✉ M/Kiti CCM: mwenyekiticcm@ccmid.in
✉ M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
✉ Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

3.0 MAFANIKIO YA TAWI

3.1 Kuanzishwa kwa Mfumo Rasmi wa Kidijitali wa Tawi

Mojawapo ya mafanikio makubwa katika kipindi hiki ni kuanzishwa kwa website rasmi ya CCM Diaspora – India.

Mfumo huu ni hatua muhimu katika mabadiliko ya Tawi kutoka katika utegemezi mkubwa wa mfumo isiyo rasmi ya mawasiliano kwenda kwenye mfumo wa kisasa unaoweza kutumika kuhifadhi, kusambaza na kuratibu taarifa za Tawi.

Website hiyo inatarajiwa kuwa moja ya nyenzo muhimu za:

- Kutangaza shughuli za Tawi;
- Kuhifadhi taarifa rasmi;
- Kuwafikia wanachama na wapenzi wa Chama;
- Kutoa taarifa za shughuli za viongozi;
- Kuwezesha usajili wa wanachama;
- Kuwezesha ufanisi na Ustadi wa zoezi la upigaji kura wa chama.
- Kuimarisha uwazi na upatikanaji wa taarifa;
- Kujenga taswira rasmi ya CCM Diaspora – India.

Kwa mtazamo wa muda mrefu, mfumo huu unaweza kuwa msingi wa kujenga Tawi la kisasa linalotumia teknolojia katika uendeshaji wa shughuli zake.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



✉ Admin: admin@ccmid.in
✉ Customer care: info@ccmid.in
✉ Katibu wa Tawi: katibuocm@ccmid.in

✉ M/Kiti CCM: mwenyekiticc@ccmid.in
✉ M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
✉ Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

3.2 Kuboresha Utunzaji wa Kumbukumbu za Tawi

Tawi limeanza kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za shughuli zake, taarifa za viongozi, wanachama, mikutano na nyaraka mbalimbali.

Hii ni hatua muhimu kwa sababu taasisi yoyote yenye ufanisi inahitaji mfumo wa kumbukumbu unaoweza:

- Ufuatiliaji wa maamuzi;
- Uwajibikaji wa viongozi;
- Tathmini ya utekelezaji;
- Uandaaji wa ripoti;
- Uhifadhi wa historia ya Tawi;
- Uendeleo wa taasisi hata pale viongozi wanapobadilika.

3.3 Kuendesha Mikutano Minne ya Viongozi

Katika kipindi cha ripoti, Tawi limefanikiwa kuendesha mikutano minne ya viongozi.

Mikutano hiyo imekuwa sehemu muhimu ya kujadili masuala ya kiutendaji, kupanga shughuli, kufuatilia maendeleo ya Tawi na kutafuta suluhisho la changamoto zinazojitokeza.

Kuendelea kwa mikutano ya viongozi kunapaswa kuimarishwa kwa kuweka mfumo wa kudumu wa:

agenda → maamuzi → mgawanyo wa majukumu → muda wa utekelezaji → ufuatiliaji → tathmini.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibu-ccm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiti-ccm@ccmid.in



M/Kiti UVCCM: mwenyekiti-uvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

3.4 Kuanzishwa kwa Uongozi wa Mashina ya Vyuo

Tawi limefanikiwa kuteua viongozi wa mashina katika vyuo mbalimbali.

Hatua hii ni muhimu sana katika kujenga mfumo wa uongozi unaofika moja kwa moja kwa wanachama.

Mashina ya Chama katika mazingira ya vyuo anapaswa kuwa kiungo kati ya:

Tawi → Chuo → Wanachama → Wanafunzi wapya → Wapenzi wa Chama.

Uimarishaji wa mashina hayo utasaidia kupunguza pengo lililopo kati ya viongozi wa Tawi na wanachama walioko kwenye vyuo.

3.5 Kuwaunganisha Wanafunzi Wapya na Tawi

Tawi limefanikiwa kuanza kuwaunganisha wanafunzi wapya wanaofika nchini India na mfumo wa CCM Diaspora – India.

Hii ni hatua muhimu kwa sababu wanafunzi wapya ni sehemu ya nguvu kazi na rasilimali ya muda mrefu ya Diaspora.

Mfumo unaopendekezwa ni kuhakikisha kila mwanafunzi mpya wa Kitanzania anayefika India anapata taarifa kuhusu:

- CCM Diaspora – India;
- Tawi analopaswa kuwasiliana nalo;
- Shina la CCM katika chuo chake;
- Mfumo wa usajili;
- Taratibu za wanachama;
- Njia za kushiriki shughuli za Tawi.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in
Customer care: info@ccmid.in
Katibu wa Tawi: katibucem@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekiticcem@ccmid.in
M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

4.0 USAJILI WA WANACHAMA

Katika kipindi hiki, Tawi limeanza rasmi kutumia mfumo wa kidijitali wa kusajili wanachama wa CCM Diaspora – India.

Jumla ya wanachama 33 wamejiunga na mfumo rasmi wa Tawi.

Hata hivyo, uchambuzi wa hali ya usajili unaonyesha yafuatayo:

Hali ya Usajili	Idadi
Wanachama wote waliojiunga kwenye mfumo	33
Waliofuata/ kukamilisha taratibu zinazohitajika	13
Bado hawajakamilisha usajili/taarifa zote	16
Wenye changamoto ya kutokamilisha ada ya mwezi	4
Target ya Tawi	200
Utekelezaji dhidi ya target	16.5%

Takwimu hizi zinaonyesha kuwa, licha ya hatua nzuri iliyopigwa katika kuanzisha mfumo, **multikio wa wanachama bado ni mdogo ukilinganishwa na lengo lililowekwa.**

Hili linalitaji kampeni maalumu ya uhamasishaji katika kipindi kijacho.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibucom@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in



M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

5.0 USAJILI KATIKA MFUMO WA CHAMA CHA MAPINDUZI TAIFA

Tawi pia limeanza kufanikisha usajili wa wanachama katika mfumo rasmi wa Chama Cha Mapinduzi kitaifa kwa kuweka kigezo cha kuwa mwanachama rasmi wa chama ndio uweze kuwa na sifa za kujiunga na Tawi.

Hatua hii ni muhimu kwa sababu Chama Cha Mapinduzi ni taasisi binafsi ambayo rasilimali yake kubwa ni watu, ikifuatiwa na fedha.

Viongozi na wanachama wameanza kusaidiwa katika mchakato wa:

1. Kujisajili;
2. Kukamilisha taarifa zinazohitajika;
3. Kuthibitisha uanachama;
4. Kulipa ada;
5. Kuendelea kuwa wanachama hai.

6.0 MAKUSANYO YA ADA ZA UANACHAMA

Katika kipindi cha ripoti, Tawi limekusanya jumla ya:

INR 2,820

ambayo ni sawa na:

TZS 78,590.80

kwa kiwango cha ubadilishaji wa tarehe ya leo (02/09/2026).

Haya ni mapato ya moja kwa moja ya uanachama na yanaonyesha mwanzo wa kujenga mfumo wa kujitegemea kifedha.

Hata hivyo, kiwango hiki cha mapato bado hakitoshelezi kugharamia mahitaji ya msingi ya Tawi.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiticc@ccmid.in



M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

7.0 MATUMIZI YA FEDHA

Katika kipindi cha ripoti, matumizi makubwa yaliyofanyika ni pamoja na gharama za kuanzisha na kuendesha mfumo wa kidijitali wa Tawi.

7.1 Hosting

Jumla ya:

INR 8,099.46

sawa na takribani **TZS 225,724.49**

Imetumika kulipia **hosting** kwa kampuni ya **HOSTING RAJA** nchini India kwa kipindi cha miaka miwili.

Aidha, Tawi limefanikiwa kupata **domain bure** kwa mwaka wa kwanza, jambo ambalo limepunguza gharama ambazo Tawi lingelazimika kuzilipa.

7.2 Uundaaji wa Website ya Tawi

Jumla ya:

TZS 469,320

Imelipwa kwa **Mr. Azaria Hosea Kilasi** kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa website rasmi ya Tawi

8.0 HALI YA FEDHA YA TAWI

Tathmini ya kifedha inaonyesha kuwa Tawi bado liko katika hatua ya awali ya kujenga uwezo wake wa kifedha.

Mapato yaliyokusanywa kupitia ada za uanachama ni:

TZS 78,590.80

Wakati gharama zilizotajwa za kuanzisha miundombinu ya kidijitali ni:

TZS 225,724.49 + TZS 469,320 = TZS 695,044.49

Hivyo, gharama za miundombinu ya kidijitali pekee zimezidi mapato ya ada zilizokusanywa kwa takribani:





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in
Customer care: info@ccmid.in
Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in
M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

TZS 616,453.69.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa takwimu hizi, Tawi halina akiba ya fedha kwa sasa na lina mzigo wa kifedha unaohitaji kushughulikiwa.

Hali hii inasisitiza umuhimu wa kuongeza usajili wa wanachama, ulipaji wa ada na kutafuta vyanzo halali na endelevu vya mapato ya Tawi.

9.0 MAWASILIANO NA UHAMASISHAJI

Tawi limefanikiwa kuwakusanya wanachama na wapenzi wa CCM katika makundi ya WhatsApp.

Kwa sasa, jumla ya wanachama na wapenzi waliokusanywa katika makundi ya WhatsApp ya Tawi ni zaidi ya watu 333.

Hii ni rasilimali kubwa ya kijamii na kisiasa ambayo, ikiwa itasimamiwa vizuri, inaweza kusaidia kuongeza kwa kiasi kikubwa:

- Usajili wa wanachama;
- Uhamasishaji;
- Mawasiliano;
- Ushiriki wa wanachama;
- Uenezi wa taarifa rasmi;
- Ujenzi wa mtandao wa CCM Diaspora – India.

Changamoto iliyopo ni kwamba idadi kubwa ya watu waliopo kwenye WhatsApp bado haijatafsirika kikamilifu kuwa idadi ya wanachama waliosajiliwa rasmi.

Kwa hiyo, pengo kati ya watu 333+ walio kwenye mitandao ya mawasiliano na wanachama 33 waliosajiliwa rasmi linapaswa kuchukuliwa kama eneo kuu la kinkakati katika kipindi kijacho.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in



M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

10.0 MAPUNGUFU NA CHANGAMOTO

10.1 Multikio Mdogo wa Usajili wa Kidijitali

Changamoto kubwa ni multikio mdogo wa wanachama katika kujisajili kidijitali kwenye mfumo wa Tawi na mfumo rasmi wa Chama Cha Mapinduzi kitaifa.

Pamoja na kuwepo kwa mfumo, bado baadhi ya wanachama hawajachukua hatua ya kujisajili.

Hii inaonyesha kuwa **kuanzisha mfumo pekee hakutoshi; mfumo unahitaji uhamasishaji endelevu na usimamizi wa matumizi yake.**

10.2 Baadhi ya Viongozi Kuchelewa Kujisajili

Baadhi ya viongozi wamechelewa kukamilisha usajili wao katika mfumo.

Hali hii ni changamoto ya kiutendaji kwa sababu viongozi wanapaswa kuwa mfano wa kwanza katika utkelezaji wa maelekezo ya Chama.

Kiongozi aslyeonekana katika mfumo wa usajili anakuwa na ugumu wa kuhamasisha wanachama wengine kufanya hivyo.

10.3 Uhamasishaji Duni Kutoka kwa Viongozi Kwenda kwa Wanachama

Tawi bado linakabiliwa na changamoto ya baadhi ya viongozi kutifikisha kikamilifu taarifa na maelekezo kwa wanachama walio chini ya maeneo yao.

Hivyo, kuna haja ya kuimarisha mfumo wa uwajibikaji kutoka ngazi ya Tawi hadi mashina.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



✓ Admin: admin@ccmid.in
✓ Customer care: info@ccmid.in
✓ Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

✓ M/Kiti CCM: mwenyekitlccm@ccmid.in
✓ M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
✓ Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

10.4 Kukosekana kwa Akaunti Rasmi ya Malipo ya Tawi

Kwa sasa Tawi halina akaunti rasmi ya benki au njia rasmi ya malipo inayotambulika kwa jina la Tawi.

Hali hii imesababisha baadhi ya malipo kufanyika kupitia akaunti binafsi ya Katibu.

Hata kama utaratibu huo umewezesha shughuli kuendelea, si mifumo bora wa taasisi kwa mtazamo wa utawala bora, uwazi, audit trail na separation of personal and institutional finances.

Hivyo, kuanzishwa kwa akaunti rasmi ya Tawi kunapaswa kuwa moja ya vipaumbele vya juu katika kipindi kijacho.

11.0 TATHMINI YA JUMLA YA UTENDAJI

Kwa ujumla, utendaji wa Tawi katika kipindi cha Juni–Agosti 2026 unaweza kutathminiwa kama kipindi cha kujenga misingi ya taasisi, zaidi kuliko kipindi cha kuvuna matokeo makubwa ya uanachama.

Mafanikio makubwa yameonekana katika:

miundombinu ya kidijitali, utawala, kumbukumbu, mikutano, uongozi wa mashina, mawasiliano na kuanza kwa mfumo wa usajili.

Hata hivyo, matokeo ya msingi ambayo yanapaswa kuwa kipimo kikuu cha uhai wa Tawi—yaani idadi ya wanachama hai, usajili kamili, ulipaji wa ada na ushiriki wa wanachama—bado yako chini ya kiwango kinachotarajiwa.

Kwa target ya wanachama 200, usajili wa wanachama 33 unatoa utekelezaji wa **16.5%** pekee.

Hivyo, Tawi linahitaji kubadilisha mkazo kutoka kwenye **kuanzisha mifumo** kwenda kwenye **kutumia mifumo hiyo kuzalisha matokeo yanayopimika.**

12.0 MIKAKATI YA TAWI KWA ROBO MWAKA INAYOFUATA

12.1 Mkakati wa Usajili wa Wanachama 200+

Tawi litaanzisha kampeni maalumu ya kufikia angalau wanachama 200 waliosajiliwa.

Kila shina litawekewa target yake kulingana na idadi ya Watanzania na mazingira ya chuo/eneo husika.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekiticc@ccmid.in



M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

Mfumo utakuwa:

Target ya Tawi → Target ya mashina → Target ya viongozi → Target ya kila kiongozi
→ Ufuatiliaji wa kila mwezi.

12.2 Kampeni ya “Kiongozi Kwanza”

Kila kiongozi wa Tawi na Jumuiya zake anatakiwa kuhakikisha kwanza amekamilisha:

1. Usajili wa Kitaifa;
2. Usajili wa Tawi;
3. Taarifa zote zinazohitajika;
4. Ada zinazotakiwa.

Baada ya hapo kila kiongozi apewe jukumu la kuwafikia wanachama wengine.

Lengo ni kujenga falsafa ya:

“Usimwambie mwanachama afanye jambo ambalo wewe kama kiongozi hujalifanya.”

12.3 Mfumo wa Ufuatiliaji wa Wanachama

Tawi litaanzisha database yenye makundi yafuatayo:

- Waliosajiliwa kikamilifu;
- Waliosajiliwa lakini hawajakamilisha taarifa;
- Waliokamilisha usajili lakini hawajalipa ada;
- Wanachama hai;
- Wanachama wasio hai;
- Wapenzi ambao bado hawajawa wanachama rasmi.

Hii itawezesha Tawi kufanya **data-driven membership management** badala ya kutegemea makadirio.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



- Admin: admin@ccmid.in
- Customer care: info@ccmid.in
- Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

- M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in
- M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
- Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

12.4 Kubadilisha Wafuasi 333+ Kuwa Wanachama Hai

Watu zaidi ya 333 waliopo kwenye makundi ya WhatsApp watachukuliwa kama **membership conversion pool**.

Tawi litandesha kampeni maalumu ya kuwaeleza:

- Faida za uanachama;
- Taratibu za usajili;
- Umuhimu wa kulipa ada;
- Jinsi ya kutumia mfumo wa kidijitali;
- Nafasi ya mwanachama katika shughuli za Tawi.

Lengo si kuongeza idadi ya watu kwenye WhatsApp pekee, bali kubadilisha uwepo wa kidijitali kuwa ushiriki rasmi wa Chama.

12.5 Kuimarisha Mashina ya Vyuo

Kila shina la chuo litapewa:

- Kiongozi anayehusika;
- Orodha ya wanachama;
- Target ya usajili;
- Target ya uhamasishaji;
- Ratiba ya mikutano;
- Ripoti ya kila mwezi.

Viongozi wa mashina watatakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Tawi kwa vipindi maalumu ambavyo ofisi ya katibu itaitangaza.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in



Customer care: info@ccmid.in



Katibu wa Tawi: katibuoccm@ccmid.in



M/Kiti CCM: mwenyekitioccm@ccmid.in



M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in



Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

12.6 Kuanzisha Akaunti Rasmi ya Tawi

Tawi litaweka kipaumbele katika kuanzisha akaunti rasmi ya kifedha ya Tawi au mfumo mwingine wa malipo unaotambulika rasmi na unaoweza kutoa kumbukumbu sahihi za miamala.

Lengo ni:

- Kuondoa utegemezi wa akaunti binafsi;
- Kuimarisha uwazi;
- Kutenganisha fedha binafsi na fedha za Tawi;
- Kurahisisha auditing;
- Kujenga imani kwa wanachama na viongozi.

12.7 Mfumo wa Bajeti na Financial Controls

Kuanzia kipindi kijacho, Tawi linapaswa kutumia mfumo wa:

Budget → Collection → Expenditure → Reconciliation → Financial Report.

Kila matumizi ya Tawi yanapaswa kuwa na kumbukumbu, uthibitisho na uhalali wa kiutendaji.

12.8 Kuanzisha Mfumo wa Kadi/Kitambulisho cha kidigital cha tawi

Katibu wa Tawi Ndg Is-haka Rashid Hadid, atapeleka mapendekezo kwenye vikao rasmi cha viongozi, na kuangalia uwezekano wa kuwa na mfumo wa utambulisho wa wanachama unaoweza kuhusishwa na database ya Tawi.

Hii itasaidia kujenga database yenye taarifa sahihi na kupunguza tatizo la taarifa zilizokosekana.

12.9 Mikutano ya Kawaida ya Viongozi

Mikutano ya viongozi iendelee kwa utaratibu maalumu, lakini kila mkutano uwe na:

Agenda → Minutes → Resolutions → Action Points → Responsible Person → Deadline → Follow-up.

Hii itabadilisha mikutano kutoka kuwa sehemu ya majadiliano pekee na kuwa mfumo wa usimamizi wa utekelezaji.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in
Customer care: info@ccmid.in
Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekitiocm@ccmid.in
M/kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

12.10 Mfumo wa Tathmini ya Utendaji wa Viongozi

Tawi litaweka mfumo wa kupima utendaji wa viongozi kwa kutumia viashiria vinavyopimika, kama vile:

- Idadi ya wanachama waliosajiliwa;
- Idadi ya wanachama waliokamilisha taarifa;
- Ada zilizokusanywa;
- Mikutano iliyofanyika;
- Wanachama waliofikiwa;
- Shughuli zilizotekelezwa;
- Ripoti zilizowasilishwa.
- Mahudhurio ya vikao rasmi.

Hii itasaidia kujenga utamaduni wa uwajibikaji wa matokeo (**results-based leadership**).

13.0 VIPAUMBELE VIKUU VYA TAWI

Kwa kuzingatia hali ya sasa, vipaumbele vitano vikuu vya Tawi katika kipindi kijacho vinapaswa kuwa:

Kwanza: Kuongeza usajili kutoka wanachama 33 kuelekea target ya 200+.

Pili: Kukamilisha usajili wa wanachama ambao bado hawajakamilisha taarifa zao.

Tatu: Kuongeza ulipaji wa ada na kujenga msingi wa kujitegemea kifedha.

Nne: Kuanzisha akaunti rasmi ya Tawi na mfumo madhubuti wa usimamizi wa fedha.

Tano: Kuimarisha mashina na kuwawajibisha viongozi katika uhamasishaji wa wanachama.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in
Customer care: info@ccmid.in
Katibu wa Tawi: katibu@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in
M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in
Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

14.0 HITIMISHO

Robo mwaka ya pili ya mwaka 2026 imekuwa kipindi muhimu katika historia ya CCM Diaspora – India kwa sababu Tawi limeanza kujenga miundombinu yake rasmi ya kiutawala, kidijitali na kiuendeshaaji.

Kuanzishwa kwa website rasmi, kuboreshwa kwa utunzaji wa kumbukumbu, kuendesha mikutano ya viongozi, kuteua viongozi wa mashina ya vyuo, kuwaunganisha wanafunzi wapya, kuanza usajili wa kidijitali na kuanza ukusanyaji wa ada ni hatua muhimu zinazoweka msingi wa Tawi imara na endelevu.

Hata hivyo, mafanikio hayo hayawezi kuwa na maana kamili ikiwa hayatafuatiwa na ongezeko kubwa la wanachama hai, ulipaji wa ada, ushiriki wa viongozi na uwajibikaji wa pamoja.

Takwimu za sasa zinaonyesha wazi kuwa bado kuna kazi kubwa mbele yetu. Wanachama 33 pekee kati ya target ya 200 ni 16.5%, wakati zaidi ya watu 333 tayari wamekusanywa katika mitandao ya mawasiliano ya Tawi.

Hivyo, changamoto kubwa iliyopo si ukosefu wa watu wa kuwafikia, bali ni kuwageuza watu waliopo katika mtandao wa mawasiliano kuwa wanachama waliosajiliwa, waliokamilisha taarifa zao, wanaolipa ada na wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za Chama.

Kwa upande wa fedha, Tawi bado halina akiba na lina mzigo wa gharama uliojitokeza katika ujenzi wa miundombinu yake ya awali. Hivyo, Tawi haliwezi kutegemea mtu mmoja au viongozi wachache kuendesha shughuli zake.

Ni muhimu kuelewa kwamba:

TAWI NI LA WANACHAMA WOTE.
TAWI SI LA KIONGOZI MMOJA.
TAWI NI JUKUMU LA PAMOJA.

Uhai wa Tawi hautategemea M/kiti pekee au Katibu pekee, au kiongozi mwingine mmoja; utategemea kiwango ambacho kila kiongozi, kila mwanachama na kila mpenzi wa Chama atashiriki katika kulijenga.

Kwa hiyo, kipindi kijacho kinapaswa kuwa kipindi cha utekelezaji wenye matokeo, ambapo kila kiongozi atakuwa na jukumu linalopimika na kila mwanachama atahamasishwa kuchukua hatua.





CHAMA CHA MAPINDUZI

TAWI LA INDIA

Umoja, Imani na Ushindi



Admin: admin@ccmid.in

Customer care: info@ccmid.in

Katibu wa Tawi: katibuccm@ccmid.in

M/Kiti CCM: mwenyekiti@ccmid.in

M/Kiti UVCCM: mwenyekitiuvccm@ccmid.in

Katibu UVCCM: katibu-uvccm@ccmid.in

Tawi linatoa wito kwa viongozi na wanachama wote kuendelea kushirikiana, kuhamasishana, kujisajili, kulipa ada na kushiriki katika shughuli za Chama ili kujenga CCM Diaspora – India yenye nguvu, mshikamano, uwazi, uwajibikaji na uwezo wa kujitegemea.

“Tawi ni letu sote; kulijenga ni wajibu wetu sote.”

15.0 TAMKO LA MWISHO LA KATIBU

Kwa niaba ya uongozi wa Tawi, linaloongozwa na M/kiti wa Tawi **Prof Ben Anania Tweve** ninawashukuru viongozi wote, wanachama na wapenzi wa Chama kwa ushirikiano wao katika kipindi hiki.

Pamoja na changamoto zilizopo, msingi muhimu tayari umewekwa. Kazi inayofuata ni kuhakikisha kwamba msingi huo unazalisha matokeo yanayoonekana.

Tushirikiane.

Tujisajili.

Tulipe ada.

Tushiriki.

Tuwafikie wengine.

Na kwa pamoja tulijenge Tawi letu.

CCM DIASPORA – INDIA: TAWI NI LETU SOTE.

Link ya Kujisajili: <https://ccmid.in/sw/register>

Imeandaliwa na:



IS-HAKA RASHID HADID

KATIBU MKUU- CHAMA CHA MAPINDUZI INDIA

02/09/2026

